



**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA KUENZISHA SHIRIKA LA MAGAZETI
YA SERIKALI, NAM. 11 YA 2008 NA KUTUNGA UPYA SHERIA YA
SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR KWA MADHUMUNI YA
KUENDESHA BIASHARA YA MAGAZETI NA KUWEKA
MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

MPANGILIO WA VIFUNGU

VIFUNGU

MAELEZO

**SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI
KUENZISHWA KWA SHIRIKA**

3. Kuanzishwa kwa Shirika.
4. Muhuri na nembo ya Shirika.
5. Malengo ya Shirika.
6. Kazi za Shirika.

**SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA SHIRIKA**

7. Uanzishwaji na muundo wa Bodi.
8. Sifa za Mwenyekiti.
9. Kazi za Bodi.
10. Uwezo wa Bodi.
11. Mwenendo wa vikao ya Bodi.
12. Katibu wa Bodi.



13. Uteuzi wa Mhariri Mwendeshaji.
14. Kazi za Mhariri Mwendeshaji.
15. Idara, vitengo na divisheni.
16. Wafanyakazi wa Shirika.

**SEHEMU YA NNE
KUENZISHWA KWA MAGAZETI YA SHIRIKA**

17. Magazeti ya Shirika.
18. Sera ya Biashara na Uhariri wa Shirika.
19. Uuzaji na usambazaji wa magazeti.
20. Biashara ya vifaa vya kuandikia, vifaa vya ofisi na huduma za uchapishaji.
21. Mtambo wa uchapaji.

**SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA FEDHA**

22. Fedha na rasilimali za Shirika.
23. Bajeti ya Shirika.
24. Hesabu na ukaguzi.
25. Ufunguaji wa hesabu za benki.

**SEHEMU YA SITA
MASHARTI MENGINEYO**

26. Kutangaza shughuli za Serikali kwenye gazeti.
27. Wajibu wa Shirika kwa Jamii.
28. Kanuni.
29. Kufuta na kubakiza.

JADWELI



SHERIA NAM. 3 YA 2026

NIMESAINI

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI**

.....**19/10**....., 2026

**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA KUENZISHA SHIRIKA LA MAGAZETI
YA SERIKALI, NAM. 11 YA 2008 NA KUTUNGA UPYA SHERIA YA
SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR KWA MADHUMUNI YA
KUENDESHA BIASHARA YA MAGAZETI NA KUWEKA
MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

**SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI**

Jina fupi na
kuanza
kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Shirika la Magazeti Zanzibar, 2026 na itanza kutumika mara baada ya kutiwa saina na Rais.

Ufafanuzi.

2. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

“Bodi” maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7(1) cha Sheria hii;

“gazeti” maana yake ni aina ya maudhui yoyote inayoandaliwa na kuchapishwa au kutolewa mtandaoni na Shirika kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na yaliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria husika;



“habari” maana yake ni taarifa kuhusu matukio ya karibuni yanayotokea ndani au nje ya nchi au ndani ya eneo maalumu la shughuli;

“jarida” maana yake ni chapisho linalotolewa kwa vipindi maalumu likiwa na makala, taarifa, habari, uchambuzi au taarifa za kitaalamu kuhusu mada mbalimbali;

“Magazeti ya Shirika” maana yake ni magazeti yaliyoanzishwa chini ya kifungu cha 17(1) cha Sheria hii;

“Mhariri Mwendeshaji” maana yake ni Mhariri Mwendeshaji wa Shirika aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 13(1) cha Sheria hii;

“Mwenyekiti” maana yake ni Mwenyekiti wa Bodi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 7(1) (a) cha Sheria hii;

“Rais” maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

“Serikali” maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

“Shirika” maana yake ni Shirika la Magazeti Zanzibar lililoanzishwa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria hii; na

“Waziri” maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya habari.

SEHEMU YA PILI KUENZISHWA KWA SHIRIKA

Kuanzishwa
kwa
Shirika.

3.-(1) Kunaanzishwa Shirika litakalojulikana kama Shirika la Magazeti Zanzibar.

(2) Shirika litakuwa ni chombo kinachojitegemea, chenye urithi wa kuendelea, chenye muhuri na kwa jina lake, kwa mujibu wa sheria yoyote husika, kitakuwa na uwezo wa:

- (a) kushitaki na kushitakiwa;
- (b) kupata, kumiliki, kununua au kuondoa mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;
- (c) kuingia katika mkataba au muamala wowote;



(d) kukopa kiwango chochote cha fedha kutoka taasisi yoyote ya fedha; na

(e) kutekeleza au kufanya jambo lolote ambalo Shirika kwa asili yake linaweza kulitekeleza kwa mujibu wa sheria.

Muhuri na
nembo ya
Shirika.

4.-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Shirika katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo katika waraka wowote wa Shirika yatathibitishwa kwa saina ya Mhariri Mwendeshaji au afisa mwingine yeyote aliyeidhinishwa na Mhariri Mwendeshaji.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Shirika utawekwa muhuri wa Shirika na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Malengo ya
Shirika.

5. Malengo ya Shirika yatakuwa ni kuwa:

(a) kituo cha biashara ya huduma za habari na biashara zinazolingana;

(b) kituo cha maudhui bora yanayojumuisha habari za uchunguzi na zenye maslahi ya umma; na

(c) kiungo baina ya Serikali na umma.

Kazi za
Shirika.

6. Kazi za Shirika ni:

(a) kuchapisha na kusambaza magazeti;

(b) kuchapisha matangazo na makala;

(c) kufanya biashara ya vifaa vya kuandikia, vifaa vya ofisini na huduma za uchapishaji;

(d) kutangaza na kusambaza sera na mikakati ya Serikali; na

(e) kufanya kazi nyengine yoyote inayohusiana na au muhimu kwa ajili ya kutekeleza masharti ya Sheria hii.



SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA SHIRIKA

Uanzishwaji
na muundo
wa Bodi.

7.-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika ambayo itaundwa na:

- (a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;
- (b) Mhariri Mwendeshaji;
- (c) Mkurugenzi anayehusika na huduma za habari;
- (d) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu;
- (e) mwakilishi kutoka Jumuiya ya Wanahabari mwenye taaluma ya uandishi wa habari, mawasiliano ya umma au fani nyengine yoyote inayohusiana na uandishi wa habari;
- (f) mwakilishi kutoka Jumuiya ya Kitaifa ya Wafanyabiashara Zanzibar ambaye ni mtaalamu wa uchumi, fedha, biashara au fani nyengine yoyote inayofanana nazo; na
- (g) mtu mwenye uzoefu katika huduma za uchapaji.

(2) Wajumbe chini ya aya ya (d), (e), (f) na (g) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na wakuu wa taasisi husika kwa kuzingatia sifa, uzoefu na jinsia zao.

Sifa za
Mwenyekiti.

8. Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ikiwa mtu huyo ana:

- (a) angalau shahada ya kwanza katika fani yoyote inayohusiana na vyombo vya habari, uchumi au biashara kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali;
- (b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba katika huduma za habari au biashara; na
- (c) uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za
Bodi.

9. Kazi za Bodi ni:

- (a) kusimamia masuala yanayohusu Shirika na utekelezaji wa kazi zake;
- (b) kutoa miongozo ya kimkakati kwa Shirika;



- (c) kumshauri Waziri juu ya masuala ya Shirika;
- (d) kusimamia utekelezaji wa sera za Shirika;
- (e) kuidhinisha fedha, rasilimali na uwekezaji unaofanywa na Shirika; na
- (f) kufanya kazi nyengine yoyote ambayo inaweza kuwa ni muhimu kwa ajili ya kufikia malengo ya Shirika.

Uwezo wa
Bodi.

10. Bodi itakuwa na uwezo wa:

- (a) kumuelekeza Mhariri Mwendeshaji kuipatia taarifa yoyote, ripoti au waraka mwengine ambao Bodi itaona ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake;
- (b) kuidhinisha:
 - (i) bajeti, mpango kazi na sera za Shirika;
 - (ii) Kanuni za Wafanyakazi na Kanuni za Fedha;
 - (iii) ada na tozo kwa ajili ya huduma zinazotolewa na Shirika;
- (c) kupendekeza muundo wa utumishi wa Shirika;
- (d) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wafanyakazi wa Shirika; na
- (e) kuajiri wafanyakazi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

Mwenendo
wa vikao
vya Bodi.

11. Masharti kuhusiana na mwenendo wa vikao vya Bodi yatakuwa kama ilivyoielezwa katika Jadwali la Sheria hii.

Katibu
wa Bodi.

12.-(1) Bodi itateua afisa wa Shirika kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu wa Bodi ikiwa mtu huyo ana:

- (a) angalau shahada ya kwanza ya fani ya sheria au mwenye sifa ya Katibu wa Shirika kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali; na
- (b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika utumishi wa umma.



(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na:

- (a) kwa kushauriana na Mwenyekiti, ataandaa ajenda za vikao vya Bodi;
- (b) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;
- (c) atatumiza kumbukumbu sahihi na zinazojitosheleza za Bodi;
- (d) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe; na
- (e) atatekeleza jukumu jengine lolote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Uteuzi wa
Mhariri
Mwendeshaji.

13.-(1) Kutakuwa na Mhariri Mwendeshaji wa Shirika ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mhariri Mwendeshaji ikiwa mtu huyo:

- (a) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya mawasiliano ya umma, uandishi wa habari au fani inayolingana nazo kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali;
- (b) ana uzoefu wa kazi ya habari kwa kipindi kisichopungua miaka saba; na
- (c) ana uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za
Mhariri
Mwendeshaji.

14.-(1) Mhariri Mwendeshaji atakuwa ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wa Shirika na atakuwa na wajibu wa kusimamia kazi za kila siku za Shirika.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mhariri Mwendeshaji:

- (a) atawajibika kwa mapato yote, matumizi na mali za Shirika;
- (b) atahakikisha wafanyakazi wa Shirika wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili na uwajibikaji;
- (c) atasimamia masuala ya nidhamu kwa wafanyakazi wa Shirika; na
- (d) atatekeleza jukumu jengine lolote kama Bodi inavyoweza kuelekeza.

Idara, vitengo
na divisheni.

15.-(1) Shirika litaanzisha idara, vitengo na divisheni kwa idadi na namna kama itakavyokuwa muhimu katika kutekeleza kazi za Shirika.



(2) Wakuu wa idara na vitengo watateuliwa na Bodi kutokana na mapendekezo ya Mhariri Mwendeshaji.

(3) Wakuu wa divisheni watateuliwa na Mhariri Mwendeshaji kwa kuzingatia sifa zao.

(4) Wakuu wa idara, vitengo na divisheni watawajibika kwa Mhariri Mwendeshaji.

Wafanyakazi
wa Shirika.

16. Kutakuwa na wafanyakazi wa Shirika watakoajiriwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

SEHEMU YA NNE KUANZISHWA KWA MAGAZETI YA SHIRIKA

Magazeti ya
Shirika.

17.-(1) Kutakuwa na magazeti ya Shirika ambayo yatasajiliwa kwa mujibu wa sheria.

(2) Magazeti ya Shirika chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki yatajumuisha:

- (a) Gazeti la Zanzibar Leo;
- (b) Gazeti la Zanzibar Mail;
- (c) Gazeti la Zaspoti; na
- (d) gazeti jengine lolote ambalo Shirika linaweza kuanzisha.

(3) Mhariri Mwendeshaji anaweza, kwa kuzingatia idhini ya Bodi, kuanzisha au kubadilisha mpangilio au muonekano wa magazeti kulingana na mahitaji ya soko.

Sera ya
Biashara na
Uhariri wa
Shirika.

18.-(1) Shirika litakuwa na sera ya biashara na miongozo ambayo inaainisha huduma za uchapaji, uuzaji wa magazeti, vifaa vya ofisi na kuandikia, matangazo au biashara nyengine yoyote ya Shirika.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Shirika litaanzisha sera yake ya uhariri kwa ajili ya kudhibiti maudhui ambayo itazingatia kanuni za maadili, misingi na viwango vya habari.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Shirika halitochapisha au kuacha kuchapisha maudhui yoyote kwa misingi ya vitisho au ushawishi kutoka kwa mtu yeyote.



Uuzaji na
usambazaji
wa magazeti.

19.-(1) Shirika litaanzisha mfumo wa kuuza na kusambaza magazeti utakaowafikia wateja kwa sehemu kubwa ndani na nje ya Tanzania.

(2) Shirika linaweza, pamoja na mfumo wa kusambaza magazeti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kuanzisha usambazaji wa magazeti kwa njia ya mtandao.

Biashara ya
vifaa vya
kuandikia,
vifaa vya ofisi
na huduma za
uchapishaji.

20. Shirika, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 6 cha Sheria hii, litajihusisha na biashara ya vifaa vya kuandikia, vifaa vya ofisi na huduma za uchapaji.

Mtambo wa
uchapaji.

21. Shirika linaweza kumiliki na kuendesha mtambo wake wa uchapaji kwa ajili ya kuchapisha magazeti na shughuli nyengine zinazohusiana.

SEHEMU YA TANO MASHARTI YA FEDHA

Fedha na
rasilimali
za Shirika.

22. Fedha na rasilimali za Shirika zitajumuisha:

- (a) kiwango cha fedha kama kinavyoweza kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;
- (b) ruzuku, zawadi, msaada, michango au mikopo kama Shirika linavyoweza kupokea kutoka kwa mtu au taasisi yoyote;
- (c) ada na tozo kutokana na huduma zinazotolewa na Shirika; na
- (d) fedha nyengine yoyote ambayo inaweza kupatikana kihalali na Shirika.

Bajeti ya
Shirika.

23.-(1) Mhariri Mwendeshaji, kila mwisho wa mwaka wa fedha, atawasilisha kwa Bodi, kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa, makadirio ya mapato na matumizi ya Shirika kwa mwaka unaofuata wa fedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Fedha na Usimamizi wa Umma, Nam. 12 of 2016.

(2) Bodi, baada ya kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Shirika itayawasilisha kwa Waziri.

Hesabu na
ukaguzi.

24.-(1) Shirika litaweka na kutunza kwa usahihi vitabu vya hesabu ambavyo vinajumuisha kumbukumbu zote za fedha na miamala kwa kila mwaka wa fedha.



(2) Mhariri Mwendeshaji, katika kila mwaka wa fedha, ataandaa au ataagiza kuandaliwa:

- (a) taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za mwaka wa fedha husika;
- (b) taarifa ya mali na madeni ya Shirika hadi kufikia siku ya mwisho ya mwaka wa fedha kwa ajili ya kuwasilishwa na kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mkaguzi mwingine yeyote aliyeteuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na
- (c) taarifa nyengine yoyote ya fedha kama ilivyoielezwa na sheria.

Ufunguaji
wa hesabu
za benki.

25. Shirika litafungua hesabu ya benki kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

SEHEMU YA SITA MASHARTI MENGINEYO

Kutangaza
shughuli za
Serikali
kwenye
gazeti.

26.-(1) Taasisi zote za Serikali zitachapisha matangazo kuhusu shughuli za taasisi zao katika magazeti ya Shirika.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, taasisi za Serikali zinaweza kutoa tangazo lake katika gazeti jengine lolote.

(3) Shirika litatayarisha miongozo kuhusu matangazo kutoka kwa taasisi za umma.

Wajibu wa
Shirika
kwa Jamii.

27. Shirika, kwa kuzingatia sheria husika, litaandaa Mkakati wa Kuwajibika kwa Jamii kwa mujibu wa biashara zake.

Kanuni.

28. Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na
kubakiza.

29.-(1) Sheria ya Kuanzisha Shirika la Magazeti ya Serikali, Nam. 11 ya 2008 inafutwa.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa au lingepaswa kufanywa chini ya sheria iliyofutwa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, litachukuliwa kuwa limefanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.



JADWELI

MWENENDO WA VIKAO VYA BODI [Chini ya kifungu cha 11]

Makamu
Mwenyekiti.

1. Wajumbe wa Bodi watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Muda wa
wajumbe.

2. Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao
vya Bodi.

3.-(1) Bodi itakutana kikawaida kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana muda wowote itakapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti na ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao cha Bodi na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

4. Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wataunda akidi katika kikao chochote cha Bodi.

Uamuzi
wa Bodi.

5. Uamuzi wa Bodi utafanywa kwa maafikiano, endapo hakuna maafikiano, uamuzi utafanywa kwa wingi wa kura na endapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

Taratibu
za vikao.

6. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kujipangia taratibu zake wenyewe kuhusiana na vikao na uendeshaji mzuri wa shughuli zake.

Mjumbe
mualikwa.

7. Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye sio mjumbe wa Bodi kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya kikao cha Bodi kama mtaalamu lakini mtu huyo aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kamati
za Bodi.

8. Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi maalumu kama itakavyoona inafaa.

Kumbukumbu
za vikao vya
Bodi.

9. Kumbukumbu za vikao vya Bodi zitathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na kutiwa saini na Mwenyekiti na Katibu.



Kukasimu
kazi za
Bodi.

10.-(1) Bodi inaweza, itakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Kamati za Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji bora wa kazi.

Kubainisha
maslahi.

11.-(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kuzingatiwa na Bodi, haraka iwezekanavyo baada kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utawekwa katika kumbukumbu za kikao, na mjumbe aliyebainisha:

(a) hatohudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya uamuzi; au

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya uamuzi.

Kusita
kuwa
mjumbe.

12. Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejuzulu;

(b) ikiwa hatohudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya afya ya kimwili au kiakili;

(d) ikiwa atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyomteua mjumbe huyo;

(e) ikiwa atasimamishwa na Waziri akishindwa kutimiza matarajio ya Mamlaka; au

(f) amefariki.

Posho la
wajumbe
wa Bodi.

13. Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watasitahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.



UMEPITISHWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 10 Septemba, 2026.


.....
(HASSAN ALI HAJI)

Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.



**AN ACT TO REPEAL THE ESTABLISHMENT OF THE CORPORATION OF
GOVERNMENT NEWSPAPERS ACT, NO. 11 OF 2008 AND RE-ENACT
THE ZANZIBAR NEWSPAPERS CORPORATION ACT FOR THE
PURPOSE OF OPERATING NEWSPAPER BUSINESS
AND PROVIDE FOR OTHER MATTERS
RELATED THERETO**

ARRANGEMENT OF SECTIONS

SECTIONS

TITLE

**PART ONE
PRELIMINARY PROVISIONS**

1. Short title and commencement.
2. Interpretation.

**PART TWO
ESTABLISHMENT OF THE CORPORATION**

3. Establishment of the Corporation.
4. Seal and logo of the Corporation.
5. Objectives of the Corporation.
6. Functions of the Corporation.

**PART THREE
ADMINISTRATION AND MANAGEMENT OF THE CORPORATION**

7. Establishment and composition of the Board.
8. Qualifications of the Chairperson.
9. Functions of the Board.
10. Powers of the Board.
11. Proceedings of the Board.
12. Secretary of the Board.



13. Appointment of Managing Editor.
14. Functions of the Managing Editor.
15. Departments, units and divisions.
16. Staff of the Corporation.

PART FOUR ESTABLISHMENT OF THE CORPORATION NEWSPAPERS

17. Corporate Newspapers.
18. Business and Editorial Policy of the Corporation.
19. Sale and distribution of newspapers.
20. Trade in stationery, office equipment and printing services.
21. Printing press.

PART FIVE FINANCIAL PROVISIONS

22. Funds and resources of the Corporation.
23. Budget of the Corporation.
24. Accounts and Audit.
25. Opening a bank account.

PART SIX MISCELLANEOUS PROVISIONS

26. Advertisement of the activities of the Government in the newspaper.
27. Corporate Social Responsibility.
28. Regulations.
29. Repeal and Saving.

SCHEDULE



ACT NO. 3 OF 2026

I ASSENT

{DR. HUSSEIN ALI MWINYI}
PRESIDENT OF ZANZIBAR AND CHAIRMAN OF
THE REVOLUTIONARY COUNCIL

.....19/01....., 2026

**AN ACT TO REPEAL THE ESTABLISHMENT OF THE CORPORATION OF
GOVERNMENT NEWSPAPERS ACT, NO. 11 OF 2008 AND RE-ENACT
THE ZANZIBAR NEWSPAPERS CORPORATION ACT FOR THE
PURPOSE OF OPERATING NEWSPAPER BUSINESS
AND PROVIDE FOR OTHER MATTERS
RELATED THERETO**

ENACTED by the House of Representatives of Zanzibar.

**PART ONE
PRELIMINARY PROVISIONS**

Short title and
commence-
ment.

1. This Act may be cited as the Zanzibar Newspapers Corporation Act, 2026 and shall come into operation after being assented to by the President.

Interpretation.

2. In this Act, unless the context requires otherwise:

“Board” means the Board of Directors of the Corporation established under section 7(1) of this Act;

“Chairperson” means the Chairperson of the Board appointed pursuant to section 7(1)(a) of this Act;

“Corporate Newspapers” means newspapers established under section 17(1) of this Act;



“Corporation” means the Zanzibar Corporation Newspapers established under section 3(1) of this Act;

“Government” means the Revolutionary Government of Zanzibar;

“journal” means publication released at regular intervals that includes articles, information, news, analysis or professional insights on various topics.

“Managing Editor” means the Managing Editor of the Corporation appointed under section 13(1) of this Act;

“Minister” means the Minister responsible for information;

“news” means information about recent events occurring within or outside the country or within a particular area of activity;

“newspaper” means any form of content designed and published or made available online by the Corporation in accordance with the provisions of this Act and registered in accordance with relevant laws; and

“President” means the President of Zanzibar and Chairman of the Revolutionary Council.

PART TWO

ESTABLISHMENT OF THE CORPORATION

Establishment
of the
Corporation.

3.-(1) There is hereby established a Corporation to be known as the Zanzibar Government Newspapers Corporation.

(2) The Corporation shall be a body corporate with perpetual succession, common seal, and shall, subject to any relevant law, be capable of:

- (a) suing and being sued;
- (b) acquiring, holding, purchasing or disposing of any movable or immovable property;
- (c) entering into any contract or transaction;
- (d) borrowing any such sum of money from any financial institution; and



- (e) performing or doing anything which the Corporation by its nature may perform in accordance with law.

Seal and
logo of the
Corporation.

4.-(1) There shall be the seal and logo of the Corporation in such form and manner as may be determined by the Board.

(2) The application of the seal and logo in any document of the Corporation shall be authenticated by the signature of the Managing Editor or any other officer authorized by the Managing Editor.

(3) Any document intended to be a document issued by the Corporation shall be sealed with the seal of the Corporation and shall be authenticated in accordance with the provisions of subsection (2) of this section.

Objectives
of the
Corporation.

5. The objectives of the Corporation shall be:

- (a) a centre for commercial media service and related businesses;
- (b) a centre for quality content incorporating investigative and public interest journalism; and
- (c) a link between the Government and the public.

Functions
of the
Corporation.

6. The functions of the Corporation are to:

- (a) publish and circulate newspapers;
- (b) publish advertisements and articles;
- (c) trade in stationary, office equipment, and printing services;
- (d) publish and disseminate Government Policies and strategies; and
- (e) perform any other function related to or necessary for carrying into effect the provisions of this Act.

PART THREE ADMINISTRATION AND MANAGEMENT OF THE CORPORATION

Establishment
and compo
sition of the
Board.

7.-(1) There shall be a Board of Directors of the Corporation which shall compose of:



- (a) a Chairperson who shall be appointed by the President;
- (b) Managing Editor;
- (c) Director responsible for information services;
- (d) State Attorney from the Attorney General's Chamber;
- (e) a representative from the Journalistic Associations qualified in journalism, mass communication or any other media related studies;
- (f) a representative from the Zanzibar National Chamber of Commerce who is an expert in economics, finance, business or any other related field; and
- (g) a person with experience in printing services.

(2) Members under paragraphs (d), (e), (f) and (g) of subsection (1) of this section shall be appointed by the Minister in consultation with heads of relevant institutions based on their qualifications, experience and gender.

Qualifications
of the
Chairperson.

8. A person shall be eligible to be appointed as Chairperson of the Board if such person has:

- (a) at least a first degree in any field related to media studies, economic or business from an institution recognized by the Government;
- (b) working experience of at least seven years in media services or business; and
- (c) high level of integrity.

Functions of
the Board.

9. The functions of the Board are to:

- (a) oversee matters relating to the administration of Corporation and the performance of its functions;
- (b) provide strategic direction to the Corporation;
- (c) advise the Minister on the affairs of the Corporation;
- (d) oversee the implementation of the policies of the Corporation;



- (e) approve funds, resources and investments made by the Corporation; and
- (f) perform any other function which may be necessary for achieving the purposes of the Corporation.

Powers of
the
Board.

10. The Board shall have powers to:

- (a) direct the Managing Editor to furnish it with any information, report or other document which the Board considers necessary for performance of its function;
- (b) approve:
 - (i) the budget, work plan and policies of the Corporation;
 - (ii) Staff Regulations and Financial Regulations;
 - (iii) fees and charges for services rendered by the Corporation;
- (c) recommend organizational structure of the Corporation;
- (d) take disciplinary action against the staff of the Corporation; and
- (e) recruit staff in accordance with the provisions of the Public Service Act, No. 2 of 2011;

Proceedings
of the Board.

11. The provisions related to proceedings of the Board shall be as prescribed in the Schedule of this Act.

Secretary of
the Board.

12.-(1) The Board shall appoint an officer of the Corporation to be the Secretary to the Board.

(2) A person shall qualify to be appointed as Secretary of the Board if such person has:

- (a) at least a first degree in law or corporate secretary from an institution recognized by the Government; and
- (b) working experience of not less than five years in public service.



(3) The Secretary of the Board shall be responsible to the Board and shall:

- (a) in consultation with the Chairperson, prepare agenda of the meetings of the Board;
- (b) take accurate minutes of the meetings of the Board;
- (c) maintain the correct and sufficient records of the Board;
- (d) give proper notification of the meetings of the Board to the members; and
- (e) perform any other duty as directed by the Board.

Appointment
of Managing
Editor.

13.-(1) There shall be a Managing Editor of the Corporation who shall be appointed by the President.

(2) A person shall qualify to be appointed as Managing Editor if such person has:

- (a) at least a first degree in mass communication, journalism or equivalent field from an institution recognized by the Government;
- (b) a working experience of not less than seven years in media; and
- (c) high level of integrity.

Functions
of the
Managing
Editor.

14.-(1) The Managing Editor shall be the Chief Executive Officer of the Corporation and shall be responsible for the day-to-day operations of the Corporation.

(2) Without prejudice to the provisions of subsection (1) of this section, the Managing Editor shall:

- (a) be accountable for all income, expenditure and properties of the Corporation;
- (b) ensure staff of the Corporation perform their responsibilities in ethical and responsible manner;
- (c) supervise disciplinary matters for staff of the Corporation; and
- (d) perform any other duty as the Board may direct.



Departments,
units and
divisions.

15.-(1) The Corporation shall establish departments, units and divisions in such numbers and manners as it may deem necessary for the fulfilment of functions of the Corporation.

(2) Heads of the departments and units shall be appointed by the Board upon the recommendation of the Managing Editor.

(3) Heads of the divisions shall be appointed by the Managing Editor based on their merit.

(4) Head of departments, units and divisions shall be accountable to the Managing Editor.

Staff of the
Corporation.

16. There shall be staff of the Corporation to be employed in accordance with the provisions of the Public Service Act, No. 2 of 2011.

PART FOUR

ESTABLISHMENT OF THE CORPORATION NEWSPAPERS

Corporate
Newspapers.

17.-(1) There shall be Corporate Newspapers which shall be registered in accordance with the law.

(2) Corporate Newspapers under subsection (1) of this section shall include:

(a) The Zanzibar Leo Newspaper;

(b) The Zanzibar Mail Newspaper;

(c) The Zaspoti Newspaper; and

(d) any such other newspaper which the Corporation may establish.

(3) The Managing Editor may, subject to approval of the Board, establish or alter the layout or appearance of the newspapers in response to the needs of the market.

Business
and Editorial
Policy of
the
Corporation.

18.-(1) The Corporation shall have business policy and guidelines that prescribe printing services, selling of newspapers, office equipment and stationary, advertisements or any other business of the Corporation.

(2) Without prejudice to the generality the provisions of subsection (1) of this section, the Corporation shall develop its own editorial policy to regulate contents which shall adhere to the journalistic code of ethics, principles and standards.



(3) Subject to the provisions of subsection (2) of this section, the Corporation shall not publish or refuse to publish any content on ground of coercion or undue influence of any person.

Sale and distribution of news papers.

19.-(1) The Corporation shall establish mechanism of selling and distribution of newspapers to cover a wide range of customers within and outside Tanzania.

(2) The Corporation may, in addition to distribution mechanism of newspaper under subsection (1) of this section, establish online newspapers distribution.

Trade in stationery, office equipment and printing services.

20. The Corporation shall, subject to the provision of section 6 of this Act, engage in trade in stationery, office equipment and printing services.

Printing press.

21. The Corporation may own and operate its own printing press for the printing of newspapers and other related activities.

PART FIVE FINANCIAL PROVISIONS

Funds and resources of the Corporation.

22. Funds and resources of the Corporation shall consist of:

- (a) such sums as may be approved by the House of Representatives;
- (b) grants, gifts, support, donations or loans as the Corporation may receive from any person or institution;
- (c) fees and charges for services rendered by the Corporation; and
- (d) any such other money that may be legally acquired by the Corporation.

Budget of the Corporation.

23.-(1) The Managing Editor shall, in respect of the end of each financial year, submit to the Board, for discussion and approval, estimates of revenue and expenditure of the Corporation for the following financial year in accordance with the provisions of the Public Finance Management Act, No. 12 of 2016.

(2) The Board shall, after discussing and approving the estimates of the revenue and expenditure of the Corporation, submit them to the Minister.

Accounts and Audit.

24.-(1) The Corporation shall, keep and maintain correctly the books of accounts which include all financial records and transactions for each financial year.



(2) The Managing Editor shall, in each financial year, prepare or order to be prepared:

- (a) a statement of income and expenditures for the relevant financial year;
- (b) report of the assets and liabilities of the Corporation until the last day of the financial year to be submitted and audited by the Controller and Auditor General of Government Accounts or any other auditor appointed by the Controller and Auditor General of the Government; and
- (c) any other financial statements as provided by law.

Opening
a bank
account.

25. The Corporation shall open bank account in accordance with the provisions of the Public Finance Management Act, No. 12 of 2016.

PART SIX MISCELLANEOUS PROVISIONS

Advertise
ment of the
activities of
the
Government
in the
newspaper.

26.-(1) All Government institutions shall be required to publish their advertisement regarding the activities of their institutions in the Corporation newspaper.

(2) Without prejudice to the provisions of subsection (1) of this section, the Government institutions may publish its advertisement in any other newspaper.

(3) The Corporation shall prepare guidelines in relation to advertisements from public institutions.

Corporate
Social
Responsibility

27. The Corporation shall, subject to any relevant law, develop its Corporate Social Responsibility Strategy in accordance with its business.

Regulations.

28. The Minister may make regulations for the better implementation of the provisions of this Act.

Repeal and
saving.

29.-(1) The Establishment of the Corporation of Government Newspapers Act, No. 11 of 2008 is hereby repealed.

(2) Notwithstanding the provisions of subsection (1) of this section, anything done or purported to be done under the repealed Act before commencement of this Act, shall be deemed to have been done under the provisions of this Act.



SCHEDULE

PROCEEDINGS OF THE BOARD [Made under section 11]

Vice-Chair-person.	1. The Board members shall elect one of them to be a Vice Chairperson of the Board.
Tenure of the members.	2. Save for ex-officio member, the Chairperson and other members of the Board shall hold the office for a term of three years from the date of their appointment and may be eligible for re- appointment for another term only
Meetings of the Board.	3.-(1) The Board shall ordinarily meet once in every three months and may convene for extraordinary meeting at any time when need arises for the discharge of its functions. (2) The Chairperson shall preside all meetings of the Board, and on his absence, the Vice Chairperson shall preside the meeting of the Board and if the Chairperson and the Vice-Chairperson are absent, the members present shall elect one among themselves to preside the meeting.
Quorum.	4. More than half of the total number of the members shall constitute quorum at any meeting of the Board.
Decisions of the Board.	5. Decisions of the Board shall be made by consensus, where there is no consensus, the decisions shall be made by majority vote and where there is an equal vote, the Chairperson shall have a casting vote.
Procedures of the Board.	6. Subject to the provisions of this Act, the Board shall have a power to regulate its own procedures in respect to the meetings and proper conduct of its activities.
Co-opted member.	7. The Board may co-opt any person who is not a member of the Board to attend in any deliberation of the meeting of the Board as an expert but the co-opted member shall have no right to vote.
Committees of the Board.	8. The Board may, for the purpose of facilitating the performance of its functions, establish committees to perform specific functions as may deem necessary.



Minutes of the meetings of the Board.

9. The minutes of the meetings of the Board shall be confirmed by the Board at the next meeting and signed by the Chairperson and secretary.

Delegation of the functions of the Board.

10.-(1) The Board may, if deems fit for the proper discharging of its functions, delegate some of its functions to the committee of the Board.

(2) Where the Board delegates its functions under subsection (1) of this section, it shall give directives in writing as may be necessary to ensure the proper performance of the functions.

Disclosure of the interest.

11.-(1) The member of the Board who has direct or indirect personal interest in a matter being considered or about to be considered by the Board shall, as soon as possible after the relevant facts have come to his knowledge, disclose the nature of his interest, at the beginning of the meeting of the Board.

(2) A disclosure of interest under subsection (1) of this section, shall be recorded in the minutes of the meeting and the member making such disclosure shall not:

- (a) be present during the deliberation of the Board for the making of the determination; or
- (b) influence any other member in the making the determination

Cessation of member ship.

12. The member shall cease to hold office upon the occurrence of the following:

- (a) resignation;
- (b) if is absent without reasonable excuse for three consecutive meetings of the Board;
- (c) if he becomes incapacitated to perform his duties by reasons of physical or mental health;
- (d) if he ceases to be a representative of the institution which nominated that member;
- (e) if he is terminated by the Minister where he does not meet the expectation of the Authority; or
- (f) death.



Allowances
of the
members
of the Board.

13. The Chairperson and other members of the Board shall be entitled to be paid such allowances in accordance with the Public Service Act, No 2. of 2011.

PASSED by the House of Representatives of Zanzibar on 10th September, 2026.

.....
(HASSAN ALI HAJI)

Clerk of the House of Representatives of Zanzibar.